

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



Kumb.Na. KDC/A.3/20/54

04/09/2017

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo anawatangazia Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

**KAZI: MTENDAJI WA KIJJI DARAJA LA III (NAFASI 49)**

**SIFA ZA MWOMBAJI;**

- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo:
- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**MAJUKUMU**

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Atakuwa katibu wa Kamati /mikutano ya Kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Ataratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji

**NGAZI YA MSHAHARA NA MSHAHARA NI KUENZIA**

TGS B = TSHS. 390,000/= - HADI TSHS. 489,000/=

**KAZI: DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 5)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amehitimu kidato cha nne (IV)
- Awe na Leseni Daraja C
- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti Cha majaribio ya ufundi Daraja la II
- Awe na uzoefu wa kuendesha magari usiopungua miaka mitatu

## MAJUKUMU

- Kuenyesha gari la Serikali
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote.
- Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo
- Kufanya matengenezo madogomadogo katika gari
- Kutunza na kuandika daftari la Safari "Log-Book" kwa safari zote.

## MSHAHARA KUANZIA;-

TGOS A = TSHS 300,000/= HADI TSHS 419,000/=


## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

- Barua zote za maombi ziambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi vya elimu na taaluma vilivyothibitishwa.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Picha mbili (2) passport size za hivi karibuni
- Maelezo binafsi (Curriculum Vitae)
- Waombaji wawe na umri kati ya miaka 18 – 45
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **19/09/2017** saa 9:30 Alasiri

Barua zote zitumwe kwa:

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO  
S.L.P 2324  
KILOLO.

Tangazo hili limetolewa na:



.....  
**ALOYCE KWEZI**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**  
MKURUGENZI MTENDAJI YA WILAYA YA KILOLO  
KILOLO